

## Je, una hofu kuwa mwizi wa utambulisho amekuibia malipo yako ya ruzuku?

**Nini cha kufanya ili ujilinde.**

**Namna ya kuripoti kwa IRS na FTC.**

Unadhani malipo yako ya ruzuku ya kiuchumi yameangukia mikononi mwa mwizi wa utambulisho? Unaweza kuripoti kwa FTC na IRS kwa wakati mmoja. Fanya yafuatayo.

Tembelea [IdentityTheft.gov](https://www.identitytheft.gov), kituo cha raslimali zote cha serikali kwa watu ili kuripoti wizi wa utambulisho na kupata mpango binafsi wa kurejesha utambulisho. Bonyeza “Get started.” Ukurasa ufuatao unauliza, “Taarifa gani inaelezea vyema zaidi hali yetu?” Bonyeza mstari unaosema, “Kuna mtu aliyejaza fomu ya marejeo ya kodi ya Nchi – au aliyedai malipo ya ruzuku ya kiuchumi – kwa kutumia maelezo yangu.” Uko katika mchakato.

[IdentityTheft.gov](https://www.identitytheft.gov) itakuuliza baadhi ya maswali ili kukamilisha Hati ya Kiapo cha Wizi wa Utambulisho ya IRS (Fomu ya IRS ya 14039) kwa ajili yako, na kuiwasilisha kielektroniki kwa IRS. Unaweza kujumuisha maelezo binafsi pia, kuwaeleza IRS kwa undani kuhusu jinsi utambulisho wako ulitumika visivyo kudai malipo ya ruzuku yako ya kiuchumi. Unaweza pia kupakua nakala ya Hati ya Kiapo uliyojaza kwa kumbukumbu yako. Na, [IdentityTheft.gov](https://www.identitytheft.gov) pia itakupa mpango wa kurejesha utambulisho wako unajumuisha hatua utakazochukua ili kujilinda zaidi kutokana na wizi wa utambulisho.

Tumia [IdentityTheft.gov](https://www.identitytheft.gov) kuripoti wizi unaoshukiwa wa utambulisho tu.

Kama una masuala **mengine** kuhusiana na malipo ya ruzuku yako kiuchumi, tembelea kurasa za IRS [Kituo cha Maelezo ya Malipo ya Ruzuku ya Kiuchumi](#) na [Maswali Yanayoulizwa Sana kuhusu Kupata Malipo Yangu](#) kwa majibu ya kina, na yanayosasishwa mara kwa mara ya maswali. Unaweza kupata pia [maelezo hapa](#) kuhusu malipo ambayo IRS inaweza kuwa imetuma kwenye akaunti usiyoitambua.

Iwe unasubiri malipo yako, au hata kama malipo yamekufikia, kuwa makini na walaghai wanaojaribu kukuibia maelezo yako ya binafsi, fedha zako, au zote. Kumbuka, IRS haitakupigia, kukutumia ujumbe, kukutumia barua pepe, au kuwasiliana nawe katika mitandao ya kijamii ikiomba maelezo yako ya binafsi au maelezo ya akaunti yako ya benki – hata yanayohusiana na malipo ya ruzuku. Pia, kuwa mwangalifu na barua pepe au ujumbe wa maandishi ulio na viambatisho au viungo unaodai kuwa na maelezo maalum kuhusu malipo. Ni za uwongo, na

## **TAARIFA KUHUSU COVID – 19** **Mpango wa Ulinzi wa Kifedha kwa Mtumiaji**

zinaweza kuwa [zinaiba](#) maelezo yako ya binafsi au zinaweza kupakua [programu hasidi](#) kwenye kompyuta, kompyuta kibao au simu yako.